



# TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR



+255 771 999 997



Email: [info@tuz.go.tz](mailto:info@tuz.go.tz)  
Website: [www.tuz.go.tz](http://www.tuz.go.tz)



S.L.P 2255

## TAARIFA MAALUM KWA VITUO VYA UTANGAZAJI KUHUSU MVUA ZA EL NINO 2026

Ikiwa tunaingia katika msimu wa **mvua za Vuli** zinazotarajiwa kuanza mwezi wa Oktoba hadi Desemba 2026, Tume ya Utangazaji Zanzibar inavielekeza vituo vyote vya utangazaji ikiwemo redio, televisheni na warusha maudhui ya mitandaoni nchini kuhakikisha **vinatoa matangazo kwa wakati yenye ujumbe wa tahadhari kwa umma kuhusu matarajio ya mvua za msimu wa Vuli 2026, zinazohusishwa na hali ya El Nino.**

Kwa mujibu wa taarifa rasmi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) mvua hizo zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani ambazo zitaanza wiki ya kwanza ya mwezi wa **Oktoba 2026 na ongezeko la mvua linatarajiwa zaidi mwezi Novemba 2026.**

**Hivyo, vituo vya utangazaji vinapaswa kutoa matangazo ya tahadhari na athari za mvua hizo sambamba na kuwahimiza wananchi wanaoishi maeneo ya mabondeni, karibu na mito na maeneo mengine hatarishi kuhama katika maeneo hayo.**

Aidha, vituo vya utangazaji vina wajibu pia wa kuwahimiza wananchi kusafisha misingi ya maji machafu na kuhakikisha njia za maji hazizuiwi na taka au vitu vingine vinavyoweza kusababisha mafuriko.

Elimu kuhusu usalama wa barabarani na usafiri ni muhimu sana pamoja na kuwaasa madereva kupunguza mwendo na kufuata maelekezo ya mamlaka za usalama.

Vituo vya utangazaji vinahimizwa kutumia vipindi vya habari, matangazo ya huduma kwa umma, vipindi vya mahojiano, mijadala na njia nyingine za mawasiliano kuhakikisha ujumbe huu unawafikia wananchi kwa wakati na kwa lugha inayoeleweka.

**Vituo vinahimizwa kutumia taarifa rasmi kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kuepuka kusambaza taarifa zisizo rasmi au zisizothibitishwa kuhusu majanga yanayohusiana na mvua hizo za El nino.**

Tume ya Utangazaji Zanzibar inaendelea kuhimiza ushirikiano wa vituo vyote vya utangazaji katika kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na za wakati kuhusu hali ya hewa na tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa.

